



## TANGAZO LA UZABUNI HUDUMA YA CHAKULA NA ULINZI

Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya (CUCoM) kinarudia kutangaza zabuni ya huduma ya chakula na ulinzi kwa mwaka wa masomo 2021/2022. Waombaji wanatakiwa kutimiza vigezo vifuatavyo:-

### A. Vigezo vya jumla kwa mwombaji

- Kuwa tayari kufanya kazi katika eneo ambalo chuo kitampangia kwa matumizi ya huduma husika.
- Awe tayari kuthibitisha uwezo alionao kifedha kuendesha shughuli anayoomba kwa kuleta taarifa zake za kibenki (bank statement) za miezi mitatu ya mwisho
- Awe na leseni halali ya biashara ya huduma husika
- Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili wa kutoa huduma katika zabuni anayoomba
- Mshiriki wa zabuni anapaswa kununua nyaraka za uzabuni (tender document) kuanzia tarehe 26/10/2021 hadi 29/10/2021 saa 2:00 asubuhi – 11:00 jioni kila siku kwa gharama ya Tsh. 100,000/= Malipo yafanyike katika benki ya CRDB akaunti namba 0150421194101 na risiti ipelekwe ofisi ya uhasibu ili kupata nyaraka za uzabuni.

### B. Vigezo vya nyongeza kwa huduma ya chakula

- Awe na cheti toka mamlaka ya udhibiti na ubora (TBS) au inayohusika na chakula
- Awe tayari kuthibitisha uwezo wa kitaaluma wa kutoa huduma ya chakula
- Huduma ya chipsi na nyama choma inajitegemea

### C. Vigezo vya nyongeza kwa huduma ya ulinzi

- Awe na kampuni ya ulinzi iliyosajiliwa rasmi
- Awe na walinzi waliofuzu mafunzo stahiki ya ulinzi (Paramilitary)
- Awe na walinzi waliohakikiwa kuwa hawajahusika katika makosa ya jinai (Vetted by Police to be crime free)
- Awe na zana za kisasa za ulinzi za kumuwezesha kukabiliana na changamoto za kiusalama (Security Devices, Security alarm system, transportation)

Utaratibu wa kurejesha nyaraka za uzabuni utakuwa kama ifuatavyo:

- Nyaraka za uzabuni zirejeshwe katika ofisi ya DPAF zikiwa zimefungwa na kuandikwa zabuni ya huduma husika kabla ya tarehe 29/10/2021 saa 11:00 jioni. Maombi yatakayofika baada ya muda huo hayatapokelewa
- Maombi ya zabuni yatafunguliwa tarehe 01/11/2021 saa 5:00 asubuhi katika ukumbi wa mikutano, mbele ya waombaji wote.
- Chuo kitamtaarifu mzabuni aliyeshinda kwa maandishi na hakibanwi kutoa zabuni kwa mshindani aliyetoa bei ya chini. Pia chuo hakitawajibika kutoa sababu kwa wale watakaoshindwa kupata zabuni.